Ontario

# *Majirani, Marafiki na Jamii*

## *Njia ya Kuongea na Wanaume Watesaji*

*Majirani, Marafiki na Jamii*

*Je, una wasiwasi kuhusu mtu ambaye unahisi anamtesa mshiriki wake, lakini hujui la kufanya? Hii kipeperushi (brosha) inaelezea njia ya kutambua dalili za kuteswa na njia unazoweza kutumia unapoongea na mwanaume mtesaji kuhusu tabia yake.*

*Majirani, Marafiki na Jamii ni kampeni ya kufahamisha watu kuhusu dalili za kuteswa kwa wanawake ili watu walio karibu na mwanamke ambaye ana hatari ya kuteswa au mwanamume anaye mtesa mkewe, waweze kusaidia*

*Kila mmoja katika jumii ana wajibu wa kutoa usaidizi ili kuangamiza kuteswa kwa wanawake. Unaweza kuafikiana na mashirika ya kijamii yanayohudumia wanawake wanaoteswa au wanaume watesaji yaliyo karibu nawe ili usaidie.*

*Hii kampeni ni ushirikiano kati ya serikali ya Ontario, Shirika la Mwongozo wa Wanawake la Ontario na Mabingwa Wanaojadiliana kuhusu Majirani, Marafiki na Jamii, kupitia kwa Kituo cha Utafiti na Elimu Kuhusu kuteswa kwa Wanawake na Watoto.*

## Dalili za Utesaji

Huenda unashuku kuwa jirani, rafiki au jamaa yako anateswa lakini hujui la kufanya au la kusema. Labda unahofia ya kuwa utaifanya hali hii kuwa mbaya zaidi. Kwa kuelewa dalili onyo za kuteswa kwa wanawake, unaweza kutoa usaidizi.

*Ukitambua dallili zifuatazo, ni vizuri uamue kuchukua hatua:*

- Mwanaume anamdharau mkewe
- Mwanaume huongea bila kumpa mkewe nafasi wala na wakati wa maongezi
- Mwanaume anamlinda au kumtafuta mkewe kila wakati hata akiwa kazini.
- Mwanaume anajipendekeza kuwa mhanga na ya kuwa ana huzuni mwingi
- Mwanaume anajaribu kuwatenganisha wewe na mkewe
- Mwanaume anamtenda mke kama mali yake
- Mwanaume hudanganya ili aonekane kuwa yeye ni mzuri au hujikuza na kujionyesha kama mwenye tabia nzuri
- Mwanaume anajifanya kuwa wa muhimu zaidi na wa thamani kuliko wote nyumbani kwake

- Mwanamke anaitetea tabia ya mmewe au anakuwa mgomvi na kukasirika
- Mwanamke anaogopa kuongea mmewe akiwepo
- Mwanamke ni anonekana kuwa mgonjwa mara nyingi na anakosa kwenda kazini
- Mwanamke anaficha majeraha yake
- Mwanamke anatoa visingizio kuhusu kwa nini hamuwezi kukutana ama anakuepuka barabarani
- Mwanamke ana huzuni, upweke, amejitenga na anauoga
- Mwanamke anatumia madawa ya kulevya au ana kunywa pombe kama njia ya kuvumilia

*(Ingawaje mara nyingi mateso ni baina ya mme na mke, pia huwezekana kutokea kati ya uhusiano baina ya mabasha na pia uhusiano baina ya wasagaji.)*

## Dalili za Hatari

*Hatari ni kubwa kama:*

- Mwanaume anaweza kumfikia mke na watoto virahisi
- Mwanaume anaweza kupata silaha kwa urahisi
- Mwanaume ana tabiya (historia) ya kutesa mkewe na wengine
- Mwanaume ametishia kumuumiza au kumuua mke kama akimuacha: Anasema "Kama hutakuwa wangu, hutakuwa wa mwingine."
- Mwanaume anatishia kuwadhuru watoto, wanyama wa nyumbani au kuharibu mali ya mkewe
- Mwanaume ametisha kujiua
- Mwanaume amempiga au amejaribu kumnyonga mke
- Mambo muhimu maishani mwa **mme** yanabadilika (kama vile kazi yake, kuachana na mkewe, kuwa na huzuni)
- Mwanaume anaamini ya kuwa mkewe amepata mwanaume mwingine

- Mwanamke ameacha au anaamua kumuacha mme
- Mwanamke anahofia maisha yake na usalama wa watoto wake **ama** haoni hatari aliyomo
- Mwanamke anawapigania watoto wake kotini au ana watoto kutoka kwa uhusiano mwingine
- Mwanamke ana uhusiano na mwingine

- Mwanaume anamlaumu mke kwa kumharibia maisha
- Mwanaume hatafuti usaidizi
- Mwanaume anamlinda mkewe na kumsikiza anapozungumza kwa simu, anasoma imeli na barua zake na anamfuata kila aendapo.
- Mwanaume ana shida ya kuwa na kazi
- Mwanaume anatumia madawa ya kulevya na anakunywa pombe kila siku
- Mwanaume haeshimu sheria

- Mwanamke na majeraha yasiyoelezeka
- Mwanamke hana njia ya kupata simu
- Mwanamke ana vikwazo ama shida zingine (kama vile kutofahamu kiingereza, si raia wa Canada, anaishi mashambani)
- Mwanamke hana marafiki wala jamaa

*Takwimu inaonyesha kuwa wanawake wa chini ya miaka 25, vilema, wa Kiaborigino na wamawake wanaoishi kimada wako katika hatari kubwa ya kuteswa. (Takwimu ya Canada: ( Mateso) kwa Familia nchini Canada. Maelezo ya Takwimu 2005)*



Wakati mwingine, watu ambao wamemzoea mwanaume mtesaji hawasemi lolote kuhusu tabia zake bali wanajihusisha na kumsaidia mwanamke anayeteswa. Wakati mwingine pia, watu wanaweza kumhurumia mtesaji na hivi basi kumfanya aendelee na utesaji wake. Kumwongeleza mwanaume mtesaji ni njia muhimu ya kuzuia kuteswa kwa wanawake, lakini kunahitaji kufanywa kwa njia angalifu. Tabia za kutesa haziwezi kuondoka bila usaidizi. Kuna hudama za kumsaidia mtesaji katika jamii anapoishi yake.

## *Haya ni mambo unaweza kufanya unapotambua dalili za utesaji:*

- Chagua wakati na mahali pazuri ili muweze kuongea kikamilifu.
- Mwendee mwanaume akiwa mtulivu
- Mweleze waziwazi kuhusu kile ambacho umeona
- Mwambia ya kwamba tabia zake ni wajibu wake. Usimpatie maoni ya kumhukumu kibinafsi. Wala usimkubalie kuwalaumu wengine kwa makosa yake
- Mwelezee ya kwamba anahitaji kuacha tabia zake.
- Usijaribu kumlazimisha kubadilisha tabia zake au kutafuta usaidizi

- Mwambie ya kwamba unahofia usalama wa mke na wa watoto.
- Usibishane na mwanaume kuhusu tabia zake za kutesa. Fahamu ya kwamba kukabiliana na kubishana na mtesaji huenda kukahatarisha zaidi hali ya yule anayeteswa
- Ita polisi iwapo usalama wa mwanamke uko hatarini.

*Mwanaume akikataa kuwa anatesa:*

- Wanaume ambao kawaida wanatesa wengine watapunguzia uzito wa makosa yao na wakatae kuwa wanayoyatenda ni mabaya. Wanaweza kusema kuwa mambo si mabaya vile au wamlaumu mwathiriwa kwa matendo yao. Tabia kama hii inageuza majukumu yao.
- Kwenye mazungumzo yako, sisitizia usalama wa familia yake na rudia tena kuwa mateso si jibu ya shida zao.
- Hakikisha kuwa kuna kuwasiliana kwa sawa na tafuta njia za kumsaidia kupata usaidizi.

*Jiweke salama wakati wote. Usijiingize kati ya vita. Wapigie polisi simu iwapo kuna hatari kubwa*

*Hii ni mifano ya mashaka ambayo utakuwa nayo iwapo unafikiri kusaidia:*

| **Hoja ya Kuwaza** | **Hoja ya Kufikiria** |
|---|---|
| Unahisi kuwa hayakuhusu | Huenda ikawa ni hali ya kufa na kupona. Vurugu inahusisha kila mtu |
| Hujui la kusema | Itakuwa ni vizuri kusema ya kuwa unajali |
| Unaweza kuharibu mambo zaidi | Mambo huenda yakawa mabaya zaidi iwapo hutafanya chochote |
| Mambo si mabaya sana yakuweza kuwahusisha polisi | Polisi wana mafunzo na njia za kutoa huduma |
| Unaogopa kuwa udhalimu wake utakugeukia wewe au jamaa zako | Muongeleshee mwanamke peke yake. Wajulishe polisi kama ukitishwa |

| Hoja ya Kuwaza | Hoja ya Kufikiria |
|---|---|
| Unadhani kuwa mwanamke hataki kuondoka kwa sababu anashinda akirudi | Huenda mwanamke hana usaidizi anaouhitaji |
| Unaogopa kuwa atakukasirikia | Labda, unadhani mwanamke atajua kuwa unajali |
| Unahisia kuwa washiriki ni marafiki zako | Rafiki mmoja anateswa na hali anaishi kwa uoga |
| Unaamini kwamba mwanamke angetaka usaidizi angeutafuta | Mwanamke anaweza kuwa na uoga mwingi na anaibika kuomba msaada |
| Unadhani ni jambo la kibinafsi | Si wakati mtu anapoumizwa |

## Habari

Nambari inayotoa msaada kwa Wanawake Wanaoteswa inaitwa Femaide: **1-877-336-2433** hutoa huduma ya simu kwa masaa 24 na pia nambari TTY **1-866- 860-7082** ya huduma kwa wanawake wa Ontario wanaoteswa na viziwi. Huduma inayotolewa ni ya kisiri kutoka kwa watu wasiojulikana.

Watoaji huduma kwa nambari hii ya simu watakuelekezea njia ya kuwasaidia wanawake wanaoteswa au wanaume wanaotesana. Watakuelezea juu ya dalili za kuteswa ambazo utakuwa umeziona na watakupatia ushauri na njia za kukuwezesha kutoa usaidizi.

Kwa habari zaidi kuhusu huduma za Nambari Saidizi ya Wanawake Wanao teswa, nenda: **www.briserlesilence.ca** Kukiwa na hali ya dharura, pigia polisi simu.

*Watu wengi wa Ontario wanahisia kuwa ni wajibu wao kibinafsi kupunguza kuteswa kwa wanawake. Wanazingatia umuhimu wa dalili za kuteswa. Kwa habari zaidi, angalia:* ***www.voisinsamisetfamilles.on.ca***

Mwezi wa tatu 2009

Inatapatikana kwa Kifaransa na lugha zingine

Imefadhiliwa na Serikali ya Ontario

SWAHILI